REVIVAL NEWS
From Revival Ministries Australia
P.O. Box 2718 BC TOOWOOMBA Q4350 Australia
Phone: 61-7-46130633; e-mail: rma@revivalministries.org.au
Website: www.revivalministries.org.au

JUNI 2020 **** JUNI 2020 **** JUNI2020

WAHUDUMU WA SIRI

Katika Wakolosai 1:24 Paulo anatupa ufahamu wa ndani kwa mwito wake wa kuwa mhudumu. Kutokana na hayo tunajifunza ni nini sehemu muhimu kwa mhudumu wa kweli wa Kristo

Mwito wa kuteseka

"Sasa nayafurahia mateso niliyo nayo kwa ajili yenu;tena nayatimiliza katika mwili wangu yale yaliyopungua ya mateso ya Kristo,kwa ajili ya mwili wake,yaani kanisa lake"wakolosai 1:24. Kitu cha kwanza ambacho Paulo anasema kuhusu huduma yake ni kiwango cha mateso aliyopitia katika kutimiza mwito wake kuwa mhudumu kwa kanisa. Mateso hayo yanaathiri mwili wa Paulo. Ni uzoefu wa kweli ambao alipitia. Wengine wanavutwa kwa huduma kwa sababu ya kazi au mapato au cheo,lakini mhudumu wa kweli wa Kristo kwanza ameitwa na mwito huo unajumuisha mateso.
Yesu alisema, "Mimi ndimi mchungaji mwema. Mchungaji mwema huutoa uhai wake kwa ajili ya kondoo" Yn.10:11.Mhudumu wa kweli ni yule 'anayetoa uhai wake kwa ndugu'. Ni mwito wa kuteseka.

Wahudumu wengine ni watu wa mshahara

Mtu anayetafuta kuingia katika huduma kwa sababu ya kibinafsi hasa ni mtu wa mshahara. Yesu alisema "mbwa-mwitu akija,mtu wa mshahara huwaacha kondoo na kukimbia. Yule hukimbia kwa kuwa ni mtu wa mshahara ;wala mambo ya kondoo si kitu kwake" Yn.10:13.

Kushughulika na makanisa

Mateso hayo huja kwa kubeba mzigo wa jukumu wa mwili. Kwa kuorodhesha mateso yake aliyoyapitia katika kutekeleza huduma yake, Paulo anasema kwamba yale yaliyompata kila siku yalikuwa "maangalizi ya makanisa yote"(2 Kor.11:28).Paulo anasema kwamba mzogo wake mkuu sio mambo magumu aliyoteseka hata kimwili, bali maangalizi yake kwa makanisa.

Ni mzigo wa maombezi

Paulo anasema kwamba mateso yake yalikuwa hasa "mateso ya Kristo".Tunajua kwamba Yesu "alipigwa,na Mungu na kuteswa"(Isaya 53:4) na tunajua kwamba mateso yake na kifo yalikuwa ridhia ya dhambi zetu. Paulo harejelei mateso ambayo Yesu hasa alitubebea, bali kunayo kwa kweli jinsi ambayo mhudumu anaweza kuingia katika mateso ya Kristo katika maombi na maombezi, kujitambulisha na roho wa Bwana kwa ajili ya mwili wake. Kumbuka ile ambayo Yesu aliteseka katika Shamba la Gethsemane haikuwa kimwili bali pengine ilikuwa ngumu zaidi kwake kubeba kuliko mateso ya kimwili ya msalaba.

Kila mwanafunzi wa kweli na kwa hakika kila mhuduma wa kweli lazima akuje kwa mahali pa kuvumilia hata wakati kuna shinikizo,mafadhaiko, dhiki na mateso ya kimwili,"siku zote

twachukua katika mwili kuuawa kwake Yesu,ili uzima wa Yesu nao udhihirishwe katika miili yetu”(2 Kor.4:8-10). Tumeitwa kupitia mambo kama hayo kwa ajili ya mwili kuachilia neema kwa mwili. (mst.15).

Uwakili wa Neema

Hudumu ni matokeo ya uwezesho wa neema. Mungu kwa roho wake hutupa uwezo wa kuhudumu (2 Kor.3:5-6).Paulo anasema kwamba “nimefanywa mhudumu wake,sawasawa na uwakili wa Mungu”(wakolosai 1:25). Huu uwakili ni uwakili wa neema. Paulo anasema katika Waefeso 3:2-3 kwamba ilikuwa “uwakili wa neema ya Mungu aliopewa” Paulo kwa ajili ya kanisa,kumwezesha kuwa mhudumu wa neno kufanya kujulikana ufunuo wa siri hiyo.
Mwito kwa huduma unaweza tu kutimizwa “kwa kadiri ya kipawa cha neema ya Mungu”(Waefeso 3:7) ambayo humwezesha mhudumu kufanya kazi ya huduma –“ni utendaji wa uweza wake”(Weafeso 3:7).
Huo mwito ni kutoka mbinguni. Yohana mbatizaji alisema “hawezi mtu kupokea neno lo lote isipokuwa amepewa kutoka mbunguni”(Yohana 3:27).

Huduma ya Neno

Uwakili kutoka kwa Mungu ni “kulitimiza neno la Mungu” (Wakolosai 1:25). Huduma ambayo tunaongea juu yake si huduma ya shemanzi, ambayo ni huduma ya utumishi, bali huduma ya neno. Mtume Petero alitoa tofauti wazi kati ya mwito wa kuhudumu neno na mwito utumishi. Katika Matendo 6:1-7 shida ya utumishi ilikuwa imetokea katika kanisa la Yerusalemu na jibu la mitume lilikuwa kuwatoa wahudumu zaidi, “ili tuwaweke juu ya jambo hili [utumishi ya utendaji] na sisi tutadumu katika kuomba na kulihudumia lile Neno”.Matokeo ya ugavi sawa wa kazi katika huduma yalikuwa “neno la Mungu likaenea,na hesabu ya wanafunzi ikazidi sana katika Yerusalemu”

KUJUA NA KUHUBIRI HIYO SIRI

Kufunuliwa kwa siri hiyo

Kulingana na Maandiko huduma ya neno inatimizwa tu wakati mhudumu akiweza kufanya kujulikana “ile siri iliyofichwa tangu zamani zote na tangu vizazi vyote”(Wakolosai 1:26). Kimaandiko,sehemu ya kimsingi ya vipawa vya huduma vya mtume na nabii ni kupokea kutoka kwa Roho Mtakatifu ufunuo wa ile siri (Waefeso 3:5) na kuifanya kujulikana kwa watakatifu. Kwa karne nyingi huduma za mtume na nabii hazijakuwepo au kama zilikuwa ,hazikupokelewa na kanisa. Kwa hivyo,kanisa halijakuwa na ujuzi wa ile siri.

Hekima ya ndani zaidi

Ile siri ni hekima ya ndani zaidi ya Mungu na ni ya wakomavu(1Kor.2:6-7). Inaweza tu kujulikana na wakomavu. Siri ile inafanywa kujulikana kwa huduma nzuri ya neno,kuleta kwa watakatifu ufunuo wa siri kwa Roho. Ujuzi wa siri ndiyo njia ambayo Mungu huwapa urithi watakatifu.

Urithi

Urithi ni “usioharibika,usio na uchafu,usionyauka,uliotunzwa mbinguni…tayari kufunuliwa wakati wa mwisho”(1Petero 1:4-5). Ujuzi wa siri huja kwa ufunuo na huo ufunuo hupewa

kwanza na Roho kwa mitume na manabii. Hiyo ndiyo sababu urejesho wa mitume na manabii ni muhimu katika nyakati hizi kwa kanisa kuja kwa ukamilifu.

Utajiri wa utukufu

Ujuzi wa siri hufanya "kuwajulisha jinsi ulivyo utajiri wa utukufu wa siri hii katika Mataifa: nao ni Kristo ndani yenu ,tumaini la utukufu"(Wakolosai 1:27).Ni ujuzi wa siri hii ndiyo hufanya kujulikana kwa ufunuo wa utukufu wa Mungu. "Mungu aliiazimu hii siri,ile hekima iliyofichwa,tangu milele,kwa utukufu wetu"(1 Kor.2:7).

Ushirika wa siri hii

Paulo alipewa neema, "kuwahubiri Mataifa utajiri wake Kristo usiopimika;na kuwaangaza watu wote wajuehabari za madaraka ya siri hiyo ,ambayo tangu zamani zote ilisitirika katika Mungu aliyeviumba vitu vyote kupitia kwa Yesu Kristo" Waefeso 3:8-9.Matokeo ya watakatifu kuja kwa ufunuo wa siri hii,ambayo ni ushirika wa ndani,ni kwamba sasa "kwa njia ya kanisa,hekima ya Mungu iliyo ya namna nyingi ijulikane na falme na mamlaka katika ulimwengu wa roho" (mst.10).

Ushindi wa kanisa

Kwa hivyo ushindi wa kanisa juu ya adui za Mungu za kiroho unategemea kanisa kuja kwa ujuzi wa siri hii na kwa hivyo tunahitaji wahudumu ambao wanaweza "kulitimiza neno la Mungu, siri hii"(Wakolosai 1:25-26), kuleta ufunuo huo kwa watakatifu,kuwezesha kanisa lote kutembea katika ukomavu. Kutembea katika ukomavu ni kutembea kwa utukufu,na hayo yote yanategemea kanisa kujua siri. Kanisa linapokuja kujua siri na kutembea katika urithi, "maarifa ya utukufu wa YAHWEH yatajaza dunia kama maji yaifunikayo bahari" Hk.2:14. Mamlaka na nguvu yatashindwa na Babiloni itaanguka! (Isa.2:2-4, Mika 4:1-4, Ufunuo 18:20).

TUNAHUDUMU VIPI?

"Ambaye sisi tunamhubiri habari zake tukimwonya kila mtu,na kumfundisha kila mtu katika hekima yote,tupate kumleta kila mtu mtimilifu katika Kristo Yesu"Wakolosai 1:28.

Kuhubiri

Dhihirisho la kwanza la huduma ya neno ni:

- Kumhubiri Kristo
- Kutangaza neno la Mungu
- Kuhubiri "utajiri wake Kristo usiopimika"(Waefeso 3:8).
- "kuhubiri habari ya kusudi lote la Mungu"(Matendo 20:27)
- Ku "enendeni ulimwenguni mwote ,mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe"(Mk.16:15)
- Ku "hubiri habari njema za ufalme wa Mungu,na jina lake Yesu Kristo"(Matendo 8:12)

Kuonya

Neno 'noutheteo'SC Gr.#3560 linamaanisha:kuweka kwa mawazo, kutahadharisha au kushutumu kwa upole na linatafsiriwa 'onya au rudi'.
Dhihirisho la pili la huduma ya neno ni:

- Kuonya kila mtu
- "kuonyana"kwa kuwa mmejazwa elimu yote (Warumi 15:14)

- Wahudumu wanafaa kuwaonya watakatifu kama sehemu ya uangalizi wao (1 Wathesalonike 5:22)
- Wale ambao hawatii neno wanafaa kuonywa kama ndugu (2 Wathesalonike 3:15)
- Neno la Mungu linapodumu ndani ya watakatifu,wanaweza "kuonyana kwa zaburi,na nyimbo,na tenzi za rohoni"(Wakolosai 3:16)
- Maandiko yameandikwa kwa maonyo yetu (1Kor.10:11)

Kufundisha

Dhihirisho la tatu la huduma ya neno ni:

- Kufundisha kila mtu
- "kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru"(Mat.28:20)
- Kufundisha "mafundisho ya kwanza ya maneno ya Mungu"(Waebrania 5:12)
- Kufundisha mafundisho ya imani hiyo (Yuda 3)
- Kufundisha mafundisho ya mitume (Matendo 2:42)
- "kufundisha habari za Bwana Yesu Kristo" (Matendo 28:31)
- "hawakukoma kufundisha na kuhubiri Yesu aliye Kristo (Matendo 5:42)

Kwa hekima yote

Dhihirisho la nne la huduma ya neno ni:

- Hekima yote
- Kristo kwetu ni "hekima ya Mungu" (1 Kor.1:24)
- Kristo "alifanywa kwetu hekima kutoka kwa Mungu" (1 Kor.1:30)
- "Bora hekima" (Mithali 4:7)
- Ni hekima kutoka juu (Yakobo 3:17)

Lengo ni ukamilifu

"tupate kumleta kila mtu mtimilifu katika Kristo Yesu" Wakolosai 1:28.

Lengo la kazi ya huduma la kila mhudumu wa mkunjo-tano (Waefeso 4:11) ni "kuwakamilisha watakatifu,hata mwili wa Kristo[wote] ujengwe,hata sisi sote tutakapoufikia …hata kuwa mtu mkamilifu,hata kufikia kwenye cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo"(Waefeso 4:12-13). Mhudumu ana jukumu kupitia kwa huduma ya neno kuwaleta watakatifu kutoka kuwa watoto (Waefeso 4:14) hadi kuwa watakatifu wakomavu,ambao wanaweza "kuishika kweli katika upendo"(mst.15) na kutenda vyema kwa "kuungamanishwa na kushikanishwa kwa msaada wa kila kiungo,kwa kadiri ya utendaji wa kila sehemu moja moja,huukuza mwili upate kujijenga wenyewe katika upendo" Waefeso 4:16.
Lengo ni utimilifu: "tukaze mwendo ili tuufikie utimilifu"(Waebrania 6:1),baada ya kuiweka misingi ya mafundisho ya kwanza "ya maneno ya Mungu"(Waebrania 5:12 &6:1-2).Watakatifu wanafaa kuwa na ujuzi "Katika neno la haki"(Waebrania 5:13).Hii itakuwa matokeo ya huduma nzuri ya neno.

Huduma ni "kadiri ya kutenda kazi Kwake"-Wakolosai 1:29

"Nami najitaabisha kwa neno lilo hilo,nikijitahidi kwa kadiri ya kutenda kazi kwake atendaye kazi ndani yangu kwa nguvu"Wakolosai 1:29.Mhudumu ameitwa 'kujitaabisha' na kujitahidi katika kazi ya huduma. Mhudumu anafaa "kujitahidi [soma] kujionyesha kuwa amekubaliwa na

Mungu, mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari,kutumia neno la kweli kwa halali”(2 Tim.2:15).
Hata hivyo,jambo muhimu katika huduma ni kujua “utenda kazi kwake”ndani mwetu (Wakolosai 1:29);Ni utenda kazi wa Mungu,nguvu ya utendaji wake ukifanya kazi ndani yetu na kupitia kwetu. Huduma inayofaa ni Mungu kutenda kupitia kwetu kwa nguvu zake na kuleta matokeo yanayoonekana. Nguvu za Mungu zinafanya kazi ndani yetu. “Basi atukuzwe yeye awezaye kufanya mambo ya ajabu mno kuliko yote tuyaombayo au tuyawezayo; kwa kadiri ya nguvu itendayo kazi ndani yetu” Waefeso 3:20.

Jibu kwa ombi la ajabu la Paulo kwetu tufanywe “imara kwa nguvu”(Waefeso 3:16); kwamba roho zetu zijae imani na kwamba tuweze kufahamu upendo wake na kujawa “na utimilifu wote wa Mungu” (Waefeso 3:17-19) linawezekana tu kwa sababu sisi ni watoto wa Mungu-nguvu zake tayari zinafanya kazi ndaniyetu! Ni nguvu hii ndiyo inafanya kazi ndani ya mhudumu,kumwezesha mhudumu “kumleta kila mtu mtimilifu katika Kristo Yesu”

Hili ndilo lengo kumleta kila kaka na dada mtimilifu[mkamilifu] katika Kristo.
“Maana tumaini letu,au furaha yetu,au taji ya kujionea fahari,ni nini? Je, si ninyi,mbele za Bwana wetu ,wakati wa kuja kwake? Maana ninyi ni utukufu wetu,na furaha yetu” 1Thes.2:19-20.

Paul Galligan.